

Je, ninapaswa kupimwa lini? Usafiri wa Kimataifa

MANUKUU

[Muziki wa kusisimua]

[Masimulizi]

Je, unapaswa kupimwa COVID-19 lini?

Familia yako inasafiri kwenda nchi nyingine. CDC inapendekeza kupimwa kabla na baada ya kusafiri. Tembelea tovuti ya CDC (<https://www.cdc.gov/coronavirus/2019-ncov/travelers/international-travel-during-covid19.html>) upate masharti ya sasa na mapendekezo ya kusafiri.

Katika baadhi ya nchi, huenda utahitajika kupimwa kabla ya kusafiri au kuhitajika kuchanjwa. Hakikisha umekagua masharti ya mahali mahususi unapoenda.

(<https://travel.state.gov/content/travel/en/traveladvisories/COVID-19-Country-Specific-Information.html>)

Zaidi ya hayo, wanaporudi Marekani, wasafiri wote **lazima** waonyeshe vipimo vinavyothibitisha kuwa hawajaambukizwa COVID-19 kilichofanywa katika muda usiozidi **siku moja** kabla ya kusafiri.

USISAFIRI ikiwa wewe ni mgonjwa au ikiwa umeambukizwa COVID-19 na bado hazijapita siku 10 tangu upate dalili au kupimwa.

USISAFIRI ikiwa ulikaribiana hivi majuzi na mtu aliye na COVID-19. Pimwa siku tano baada ya kukaribiana na mtu aliyeambukizwa, na usisafiri hadi ukamilishe karantini yako na kipindi cha siku 10 cha kujitenga.

USISAFIRI ikiwa unasubiri matokeo ya kipimo cha COVID-19. Iwapo kipimo chako kitaonyesha kuwa umeambukizwa ukiwa ulikoenda, utahitaji kujitenga na kuahirisha kurudi kwako hadi iwe salama kwako kumaliza kujitenga. Familia yako na wale uliokaribiana nao pia wanaweza kuhitaji kuwekwa karantini.

Ikiwa huna chanjo zote za COVID-19 zinazopendekezwa, hupaswi kusafiri kimataifa. Iwapo ni lazima usafiri, pimwa siku chache zaidi kabla ya kuondoka, kipindi kisichozidi siku tatu kabla ya safari yako.

Katika tukio hili, familia yako itaondoka Jumatano. Wanafamilia wote ambao hawajapata chanjo zote za COVID-19 zilizopendekezwa wanapaswa kupimwa Jumapili, Jumatatu, au Jumanne kabla ya safari yako.

Pia, *kila mtu* anapaswa kupimwa siku tatu hadi tano **baada ya** kusafiri kimataifa isipokuwa kama aliambukizwa COVID-19 katika siku 90 zilizopita.

Wewe na familia yako mtarudi kutoka safarini siku ya Ijumaa. Nyote mnapaswa kupimwa Jumatatu, Jumanne, au Jumatano. Ikiwa utapata dalili, pimwa haraka iwezekanavyo.

Wasafiri ambao hawajapata chanjo zote za COVID-19 zilizopendekezwa wanapaswa pia kukaa nyumbani (karantini) kwa siku 5 baada ya kusafiri kimataifa. Watu ambao wamepata chanjo zote za COVID-19 zinazopendekezwa au wameugua COVID-19 katika miezi mitatu iliyopita hawahitaji kuwekwa karantini.

Ili upate maelezo zaidi kuhusu nyakati nyingine unazopaswa kupimwa, na mahali pa kupimiwa, tembelea ukurasa wa tovuti ya MDH ya Kupimwa COVID-19.

(<https://www.health.state.mn.us/diseases/coronavirus/testsites/index.html>)

[Muziki wa kusisimua]

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

2/2/22 (Swahili)

Ili upate maelezo haya kwa muundo tofauti, piga simu: 651-201-4989